TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

TAARIFA YA ZOEZI LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA 2015

Tume ya Taifa ya Uchaguzi,

S.L.P 10923,

DAR ES SALAAM.

17JULY, 2015

1. Utangulizi

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura umekamilika katika Halmashauri za Mikoa ya Njombe, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Iringa Katavi, Rukwa, Mbeya, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Kagera, Simiyu, Shinyanga, Geita na Mwanza. Uandikishaji Unaendelea katika Mikoa Saba (7) ambayo ni pamoja na Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro na Pwani. Tume Inaendelea na Mafunzo ya Watendaji Zanzibar na Mkoa wa Dar es Salaam mafunzo yamekamilika.

Kazi nyingine kubwa inayoendelea ni ukamilishaji wa Mifumo na Uwekaji wa Mitambo na Mifumo ya kupokea, Kuchakata na kuhifadhi taarifa za Wapiga Kura na Taarifa nyingine mbalimbali za Uchaguzi.

Sambamba na zoezi la Uboreshahi na Ukamilishaji wa Mifumo ya Uchaguzi, Tume inaendelea na kazi mbalimbali za matayarisho ya Uchaguzi Mkuu.

2. Zoezi la Uboreshaji

Kwa ujumla Uandikishaji unaendelea vizuri kama ulivyopangwa na katika Halmashauri nyingi Uandikishaji umezidi makisio ya Wapiga Kura ambayo Tume ililenga Kuandikisha ikiwa ni pamoja na kuzidi Idadi ya watu wanaotegemewa kuwa na miaka 18 au zaidi ifikapo siku ya Uchaguzi kwa ***mujibu wa Takwimu za Sensa zilizotolewa na NBS***.

Uandikishaji katika Mikoa yote isipokuwa Dar es Salaam, Pwani na Zanzibar unaendelea kufanyika kwa kuhamisha BVR Kits mara nne ndani ya Halmashauri Moja. Ili kumaliza Uandikishaji mapema, katika Mkoa wa Pwani, Uandikishaji Utafanyika kwa kuhamisha BVR Kits mara mbili ndani ya Halmashauri zote za Mkoa wa Pwani. Dar es Salaam na Zanzibar Uandikishaji Uandikishaji umepangwa kufanyika katika vituo vyote sambamba hivyo kila Kituo kitakuwa na BVR hivyo kukamilisha Zoezi la Uandikishaji katika muda uliopangwa.

2.1 Takwimu za Uboreshaji

Takwimu za Uandikishaji katika Mikoa ambayo Uandikishaji umekamilika zimeainisha takwimu za Wapiga Kura waliokadiriwa Tume, Wananchi watakaokuwa na umri wa Miaka 18 au zaidi (kwa mujibu wa Takwinmu za NBS), Wapiga Kura walioandikishwa.

KANDA	MKOA	HALMASHAURI	MAKISIO NBS	MAKISO TUME	WALIOA NDIKISH WA	% NBS	% TUME
		NJOMBE TC	62,089	55,880	82,113	157.6	146.9
		NJOMBE DC	48,557	43,701	42,495	87.5	97.2
1		MAKETE	53,617	48,255	50,629	116.1	104.9
	NJOMBE	LUDEWA	68,512	61,661	64,908	133.8	105.3
		WANG'ING'OMBE	48,866	43,979	81,491	166.8	185.3
		MAKAMBAKO	32,370	29,133	58,692	181.3	201.5
		JUMLA	**274,011**	**246,610**	**380,328**	**138.8**	**154.2**
		NACHINGWEA DC	121,623	109,461	155,119	127.5	141.7
		KILWA DC	103,382	93,044	106,512	103.0	114.5
		RUANGWA DC	83,662	75,296	82,795	99.0	110.0
		LINDI DC	108,330	97,497	109,041	100.7	111.8
	LINDI	MANISPAA LINDI	47,356	42,620	48,850	103.2	114.6
		LIWALE DC	53,943	48,549	56,507	104.8	116.4
		JUMLA	**588,022**	**529,220**	**558,824**	95.0	**105.6**
		MTWARA MIKINDANI	72,133	64,920	84,878	117.7	130.7
		MASASI MJI	58,007	52,206	60,267	103.9	115.4
		NANYAMBA MJI	41,295	37,166	40,967	99.2	110.2
		MTWARA DC	95,908	86,317	95,209	99.3	110.3
	MTWARA	MASASI DC	146,931	132,238	146,470	99.7	110.8
		NANYUMBU	86,199	77,579	86,894	100.8	112.0
2		NEWALA	120,450	108,405	119,973	99.6	110.7
		TANDAHIMBA	150,366	135,329	134,507	89.5	99.4
		JUMLA	**773,289**	**695,960**	**769,165**	99.5	**110.5**

KANDA	MKOA	HALMASHAURI	MAKISIO NBS	MAKISO TUME	WALIOA NDIKISH WA	% NBS	% TUME
		TUNDURU DC	164,954	148,459	181,418	110.0	122.2
		NAMTUMBO DC	108,043	97,239	117,039	108.3	120.4
		SONGEA DC	98,410	88,569	99,899	101.5	112.8
		SONGEA MANISPAA	116,932	105,239	137,738	117.8	130.9
	RUVUMA	MBINGA DC	196,211	176,590	196,744	100.3	111.4
		NYASA DC	78,815	70,934	77,143	97.9	108.8
		JUMLA	**763,365**	**687,029**	**809,981**	**106.1**	**117.9**
		MANISPAA YA IRINGA	95,587	86,028	105,662	110.5	122.8
		MAFINGA MJI	48,956	44,060	48,669	113.3	110.5
	IRINGA	KILOLO	118,692	106,823	110,412	93.0	103.4
		IRINGA DC	134,165	120,749	137,950	102.8	114.2
		MUFINDI	126,191	113,572	123,323	97.7	108.6
		JUMLA	**524,390**	**471,951**	**526,016**	**101.6**	**111.5**
		BAHI	110,802	99,722	102,195	92.2	102.5
		CHAMWINO	173,811	156,430	157,545	91.0	100.7
		CHEMBA	120,887	108,798	108,602	89.8	99.8
	DODOMA	DODOMA MJINI	248,550	223,695	272,308	109.6	121.7
		KONDOA	129,424	116,482	125,937	97.3	108.1
		KONGWA	86,737	78,063	146,680	169.1	187.9
		MPWAMPWA	154,873	139,386	139,869	90.3	100.3
		JUMLA	**1,025,084**	**922,576**	**1,053,136**	**102.7**	**114.2**
		CHUNYA	151,432	136,289	183,818	121.4	134.9
		MBEYA	398,814	358,933	395,453	99.2	110.2
		KYELA	123,707	111,336	110,594	89.4	99.3
		RUNGWE	191,841	172,657	175,116	91.3	101.4
3		ILEJE	68,044	61,240	60,052	88.3	98.1
	MBEYA	MBOZI	232,470	209,223	198,982	85.6	95.1
		MOMBA	148,799	133,919	145,814	98.0	108.9
		MBARALI	162,258	146,032	147,005	90.6	100.7
		JUMLA	**1,477,365**	**1,329,629**	**1,385,634**	**93.8**	**104.2**

KANDA	MKOA	HALMASHAURI	MAKISIO NBS	MAKISO TUME	WALIOAN DIKISHWA	% NBS	% TUME
		MPANDA TC	51,000	45,900	76,065	149.1	165.7
		MPANDA DC	52,000	46,800	80,036	153.9	171.0
	KATAVI	NSIMBO	56,466	50,819	47,802	84.7	94.1
		MLELE	84,000	75,600	80,928	96.3	107.0
		JUMLA	**243,466**	**219,119**	**284,831**	**117.0**	**130.0**
		SUMBAWANGA MANISPAA	106,740	96,066	112,811	105.7	117.4
		NKASI	154,345	138,911	125,030	81.0	90.0
	RUKWA	SUMBAWANGA	129,234	116,311	128,455	99.4	110.4
		KARAMBO	99,641	89,677	92,391	92.7	103.0
		JUMLA	**489,960**	**440,964**	**458,687**	**93.6**	**104.0**
		SINGIDA MC	84,945	76,451	85,697	100.9	112.1
		MANYONI	151,619	136,457	148,584	98.0	108.9
		IKUNGI	134,106	120,695	123,245	91.9	102.1
	SINGIDA	SINGIDA DC	109,291	98,362	90,653	82.9	92.2
		MKALAMA DC	94,874	85,387	87,749	92.5	102.8
		IRAMBA DC	124,075	111,668	110,010	88.7	98.5
		JUMLA	**698,910**	**629,019**	**645,938**	**92.4**	**102.7**
		TABORA MC	134,437	120,993	139,343	103.6	115.2
		IGUNGA	184,246	165,821	178,794	97.0	107.8
		TABORA DC(UYUI)	170,123	153,111	169,075	99.4	110.4
		URAMBO	83,553	75,198	98,901	118.4	131.5
	TABORA	KALIUA	183,222	164,900	156,426	85.4	94.9
		SIKONGE	87,768	78,991	108,370	123.5	137.2
		NZEGA	239,832	215,849	233,476	97.3	108.2
		JUMLA	**1,083,181**	**974,863**	**1,084,385**	**100.1**	**111.2**
4							
		BUHIGWE	122,631	110,368	98,580	80.4	89.3
		KASULU DC	193,290	173,961	119,990	62.1	69.0
		KAKONKO	80,028	72,025	62,036	77.5	86.1
		UVINZA	187,328	168,595	118,230	63.1	70.1

	KIGOMA	MANISPAA KIGOMA UJIJI	116,187	104,568	100,210	86.2	95.8
		KIBONDO	123,466	111,119	102,189	82.8	92.0
		KASULU TC	103,400	93,060	79,578	77.0	85.5
		KIGOMA DC	105,831	95,248	94,128	88.9	98.8
		JUMLA	**1,032,161**	**928,945**	**774,941**	**75.1**	**83.4**
		BUKOBA MJNI	75,577	68,019	71,696	94.9	105.4
		BUKOBA VIJIJINI	148,033	133,230	131,876	89.1	99.0
		BIHARAMULO	145,292	130,763	127,473	87.7	97.5
		KARAGWE	167,261	150,535	118,126	70.6	78.5
	KAGERA	KYERWA	152,564	137,308	118,892	77.9	86.6
		MISSENYI	106,617	95,955	98,951	92.8	103.1
		MULEBA	275,594	248,035	248,172	90.0	100.1
		NGARA	146,450	131,805	124,082	84.7	94.1
		JUMLA	**1,217,388**	**1,095,649**	**1,039,268**	**85.4**	**94.9**
		MWANZA UJIJI	210,220	189,198	273,636	130	145
		ILEMELA	196,067	176,460	234,879	120	133
		MISUNGWI	168,076	151,268	149,535	89	99
		SENGEREMA	159,248	143,323	153,054	96	107
	MWANZA	MAGU	145,473	130,926	147,155	101	112
		UKEREWE	173,395	156,056	162,883	94	104
		KWIMBA	102,763	92,487	86,273	84	93
		SUMVE	87,993	79,194	76,466	87	97
		BUCHOSA	160,508	144,457	158,510	99	110
		JUMLA	**1,403,743**	**1,263,369**	**1,442,391**	**103**	**114**
		BUSEGA	96,183	86,565	104,365	109	121
		ITILIMA	188,400	169,560	129,637	69	76
		BARIADI TC	72,170	64,953	76,752	106	118
	SIMIYU	MEATU	128,399	115,559	128,158	100	111
		BARIADIDC	140,000	126,000	117,097	84	93
		MASWA	164,837	148,353	157,285	95	106
5		**JUMLA**	**789,989**	**710,990**	**713,294**	**90**	**100**
		USHETU	140,181	126,163	123,635	88	98
		KAHAMA MJI	105,103	94,593	149,304	142	158
		KISHAPU	120,000	108,000	126,831	106	117
	SHINYANGA	MSALALA	122,701	110,431	119,595	97	108
		SHINYANGA DC	156,859	141,173	150,788	96	107
		SHINYANGA MC	97,261	87,535	98,117	101	112
		JUMLA	**742,105**	**667,895**	**768,270**	**104**	**115**

		GEITA TC	98,653	88,788	106,336	108	120
		GEITA DC	283,894	255,505	236,324	83	92
	GEITA	BUKOMBE DC	105,385	94,847	125,737	119	133
		CHATO DC	186,394	167,755	175,386	94	105
		MBOGWE	80,878	72,790	87,110	108	120
		NYANGHWALE	67,003	60,303	84,312	126	140
		JUMLA	**822,207**	**739,986**	**785,206**	**95**	**106**
		JUMLA KUU	**13,086,603**	**11,777,943**	**12,891,143**	**99**	**109**

Katika Mikoa kumi na saba (17) ambapo zoezi la Uandikishaji limekamilika, Wapiga Kura walioandikishwa ni **12,891,143** sawa na **109%** kwa makisio ya Tume na **99%** kwa Idadi ya Wananchi watakaokuwa na umri wa miaka 18 au zaidi ifikapo siku ya Uchaguzi (***kwa mujibu wa takwimu za NBS***)

Katika Halmashauri nyingi Tume imefanikiwa kuandikisha zaidi ya **100%** ya Wananchi waliolengwa kuandikishwa.

Changamoto zinazojitokeza katika Zoezi la Uboreshaji

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, zipo pia changamoto zilizojitokeza katika zoezi la Uandikishaji katika mikoa iliyomaliza Uandikishaji na inayoandikisha sasa. Changamoto hizo zimepatiwa na zinaendelea kupatiwa ufumbuzi na Zoezi linaendelea vizuri.

Hatua iliyofikiwa katika Uandikishaji



Mabadiliko ya Mipaka ya Kiutawala

Mabadiliko ya maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (Miji na Wilaya) yaliyotangazwa katika GN No. 220 na 221 ya tarehe 5 Juni 2015 yameongeza Halmasahuri nane **(8)** na Kata mia moja na thelathini na sita **(136).** Manadiliko haya yanatakiwa kutambuliwa na Tume ya Taifa mara moja kwani Tume ipo katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Bunge na Madiwani na Halnashauri mpya zimepewa majimbo kwa mujibu wa Vigezo vya Tume. Majimbo na Kata mpya

zitatakiwa kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa ajili ya Uchaguzi wa Madiwani hivi karibuni *(Kabla ya Siku ya Uteuzi).*

Mabadiliko haya yamefanyika baada ya Tume kukamilisha zoezi la kuandaa vituo na kukamilisha *Delimitation Database* ambayo imewekwa katika Mfumo wa Uandikishaji. Mabadiliko haya yamekuja wakati baadhi ya maeneo Tume imekwisha kamilisha Uandikishaji na sehemu ngingine Uandikishaji Unaendelea hivyo yameiletea Tume changamoto zifuatazo:

i. Kuwa na mahitaji ya kupitia tena upya Vituo katika maeneo yaliyoongezwa ili kuona kama hayataleta vugugu siku ya upigaji kura. Imejitokeza mara nyingi Wapiga Kura kugomea zoezi la Uchaguzi kwa sababu ya kuwekwa katika eneo wasilolitaka na ambalo hawaishi.

ii. Kulazimika kurudia Uandikishaji au kurudia kuchapisha Kadi za Wapiga Kura katika maeneo yaliyobadilika baada ya kumaliza unadikishaji kwa kuwa Kadi za Wapiga Kura huwa na Anuani ya Makazi katika QR Code na pia huchapishwa Kata, Kijiji/Mtaa na Kituo alichojiandikisha Mpiga Kura. Maeneo ambayo yamekutwa na tatizo hili ni pamoja na Halamshauri mpya Wilaya Madaba iliyopo Ruvuma, Halmashauri ya Mji Newala iliyopo Mtwara, Halmashauri ya Wilaya Mpwimbwe iliyopo Katavi na Halmashauri ya Mji wa Kondoa iliyopo Dodoma.

iii. Kuchelewesha zoezi la Uandikishaji kwani ili kuokoa muda mwingi zaidi utakaopotea kwa kushughulikia mabadiliko ndani ya Dadatase na Kadi za Mpiga huitajika kufanya mabadiliko na kubadili delimitation Database ndani ya Mfumo wa Uandikishaji katika BVR na katika Backend System.

iv. Kuhitajika kwa vifaa zaidi kwa haraka na kutokuwa na muda wa kukamilisha taratibu za manunuzi kwa mujibu wa Sheria. Vifaa vya nyongeza vitahitaji fedha zaidi.

v. Uchoraji wa ramani kuwa mgumu kutokana na jinsi baadhi mipaka iliyoandaliwa.

Changamoto hizi ndizo zilizopelekea Tume kuomba kusimamisha zoezi la kubadili mipaka hadi hapo Uchaguzi Mkuu utakapokamilika.

3. Maandalizi ya Uandikishaji Dar es Salaam na Zanzibar

Mkoa wa Dar es Salaam una Jumla ya Kata **102** na Vituo **1,669.** Wapiga kura wanaolengwa kuandikishwa na Tume ni **2,939,637.** Uandikishaji umepangwa kufanyika kwa mara moja katika vituo vyote ambapo kila Kituo kitakuwa na BVR Kit. Hivyo BVR Kits zilizopangwa kutumika ni **1,696**. Kila Manipaa itapatiwa BVR Kit za ziada (Buffer BVR Kits) zaidi ya **75%** kwa ajili ya kuweka maeneo yenye watu wengi ili Uandikishaji uweze kukamilika kwa Siku kumi (10). Jumla ya BVR Kits zitakazotumika ni **3,100** ambazo iwapo zitatumika kwa siku kumi zitaweza kuandikisha Wapiga Kura **3,720,000.**

Tume imepanga kuongeza siku mbili za weekend ili kuweza kuwaandikisha Wafanyakazi ambao hawatapata muda wa kujiandikisha siku za kazi**. I**wapo itabidi kuongeza siku mbili idadi ya Wapiga Kura watakaoweza Kuandikishwa itakuwa **4,464,000** ukilinganisha na Idadi ya **Watu 2,932,930** Watakaokuwa wamefikisha umri wa miaka 18 ifikapo siku ya Uchaguzi (***Kwa mujibu wa takwimu za NBS zilizotolewa hivi karibuni***)

Ratiba ya Uandikishaji Kwa Dar es Salaam na Zanzibar

Na.	**Kanda/Mikoa**	**Tarehe za Uandikishaji**
1	Dar es Salaam	22/07/2015 - 31/07/2015
2	Zanzibar	22/07/2015 - 23/07/2015

Kutokana na ratiba hii Uandikishaji vituoni utakamilika tarehe 31/07/2015 .

Vifaa

Vifaa vyote muhimu vinavyotakiwa katika Uandikishaji vimeandaliwa na vitakuwepo vya kutosha wakati wa Uandikishaji. Maandalizi ya Vifaa hivyo na Idadi yake ni kama ifuatavyo.

i. BVR Kits 3,100
ii. Form No. 1 Zipo 6,000,000
iii. PVC Cards kwa ajili ya Voter ID Cards zipo 5,714,000
iv. Wino wa Printer (Ribbons) 14,600 Unaoweza kuandikisha Wapiga Kura 5,840,000
v. Cleaning Kits kwa ajili ya kuchapisha kadi 9,000,000

3.1 Uwekaji wa Wazi wa Daftari la awali la Wapiga Kura

Tume imekwisha pokea Taarifa za Wapiga Kura walioandikishwa kutoka katika Halmashauri za Mikoa ya Njombe, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Iringa Katavi, Rukwa, Mbeya, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Kagera, Simiyu, Shinyanga, Geita na Mwanza. Taarifa hizo zimekwisha ingizwa katika Kanzi ya Wapiga Kura (Database) na kuchakatwa.

Baadhi ya changamoto zimemeonekana baada ya kuchakata taarifa hizo. Changamoto hizo ni pamoja na:

1. Baadhi ya Wapiga Kura waliandikishiwa katika Training Mode hivyo kutokuwa na namba ya Mpiga Kura (Unique Number)

2. GN. No. 220 na 221 ya Mipaka ya kiutawala iliyotoka tarehe 5 Juni 2015 ilitoka wakati Tume imekwisha andikisha mikoa 13 na wakati huo ilikuwa imepangwa kuandikisha mikoa saba (7). Kwa kuwa Halmashuri 8 na Kata 136 ziliongezeka, baadhi ya taarifa za Wapiga Kura walioandikishwa katika maeneo yaliyobadilika zimeathirika.

Baadhi yake yatahitaji kutoa Kadi Mpya za Mpiga Kura katika maeneo hayo.

3. Kutokana na Uharaka wa kuleta na kusafirisha BVR Kit, Taarifa za Majaribio ya BVR Kits hazikuondolewa hivyo baadhi ya Wachina waliokuwa wanafanya majaribio ya BVR Kits kabla ya Kusafirishwa kuonekana katika Database.

4. Taarifa za Majaribio ya BVR Kits yaliyofanyika Decemba 2014 kuhitaji marekebisho mengi hususan katika picha, namba ya Mpiga Kura, Vituo n.k

5. Baadhi ya XML file kutosomeka kwa urahisi hivyo kuhitaji muda na processing power kubwa kuliko iliyopangwa kutumika. Tatizo hili linaweza kusababisha kutokuwa na baadhi ya Taarifa katika Daftari

6. Kuwa na Watu waliojiandikisha zaidi ya mara moja wengi ambao wanatakiwa kuondolewa pia kuandaa taarifa na kuikabidhi wakati wa Display.

7. Kurekebisha kasoro zilizobainika katika mfumo wa kuhamisha kwa usahihi Wapiga Kura wanaotaka kuhamisha taarifa zao

Zipo pia changamoto ndogo ndogo kama ya Networking, Processing Power, Kuunganisha Storage kwa link yenye kasi Zaidi n.k Kwa kuwa changamoto hizo zote zinatatulika, Ilipangwa kwa kadiri inavyowezekana kutatua kwa kiasi kikubwa cha changamoto hizi ili kuweka wazi Daftari ambalo litakuwa safi. Daadhi ya Changamoto hizo zinachukua Muda mrefu kutatulika na baadhi zinahitaji fedha.

Kazi kubwa imefanyika ya kuondoa kasoro zote kubwa. Changamoto zinazohusiana na mabadiliko ya Mipaka yaliyofanywa na TAMISEMI ndizo zinazohitaji muda mfefu zaidi. Pale ambapo itaonekana itabidi kurekebisha taarifa za Wapiga Kura wengi kwa kuwaandikisha upya ili kurekebisha Kadi inatafutiwa ufumbuzi.

Uchapishaji wa Daftari umekamilika katika Mikoa ya Njombe, Lindi, Mtwara, Iringa na Ruvuma. Uchapishaji Utaendelea bila kusimama katika Mikoa yote ambayo imemaliza Uandikishaji na taarifa zao kuchakatwa.

Ratiba ya Display

Na.	Mikoa	Tarehe
1.	Njombe, Lindi, Mtwara, Iringa na Ruvuma	29/07/2015 – 02/08/2015
2.	Katavi, Rukwa, Mbeya, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma na Kagera	29/07/2015 – 02/08/2015
3.	Simiyu, Shinyanga, Geita na Mwanza	04/08/2015 – 08/08/2015
4.	Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro na Pwani, Zanzibar	07/08/2015 – 11/08/2015
5.	Dar es Salaam	09/08/2015 – 13/08/2015

Itafanyika kila linalowezekana kurudisha tarehe hizi nyuma kwani impepangwa kuongeza processing Power na Memory na pia kuendelea kufanya kazi kwa masaa 24 (Usiku na Mchana)

Pamoja na jitihada za kuchapisha Daftari na kusafirisha daftari hilo kwa ajili ya Display ratiba hiyo inaweza kucheleweshwa au kutotekelezeka kwa ajili ya ukosefu wa fedha kwa upande wa Hazina. Tume ililipa fedha hizo mapema lakini hadi sasa hazijaweza kupatikana ili zitumwe katika Halamashauri.

Makundi yanayoomba Kuandikishwa wakati wa Kuweka wazi Daftari

Makundi mbalimbali yanayoomba Kuandikishwa wakati wa Kuweka wazi Daftari ambayo kwa sababu mbalimbali hawakuweza kujiandikisha wakati zoezi lilipokuwa linafanyika katika maeneo yao. Makundi hayo ni pamoja na:

1. **Wakimbizi waliopewa Uraia.** Wakati Zoezi lilipokuwa linafanyika sehemu zilizokuwa na Makambi ya Wakimbizi, Tume haikuwa na Vituo vya Uandikishaji katika makambi. Hali hii ilitokana na Ushauri wa Halmashauri husika na Kamati zao za Ulinzi na Usalama. Baada ya GN. No 220 na 221 kutoka kata ziligawanya hivyo ikatokea vijiji vilivyokuwa wanakaa Wakimbizi kuwa Kata na hivyo kutokuwa na Vituo katika baadhi ya Kata hizo. Kwa kuwa Kata zimepitishwa na Mamlaka Husika itabidi kufanyika Uchaguzi katika Kata hizo. Kwa mantiki hiyo utaona ni vema kuanzisha Vituo na Wapiga kura kuandikishwa ili kuweza kuchagua Diwani wa Kata hiyo.
2. **Wanafunzi wa Dar es Salaam:** Wakati zoezi litakapokuwa linafanyika Dar es Salaam wanafunzi wa Dar es Salaam watakuwa likizo na hawatapata fursa ya kujiandikisha. Wanafunzi wamekuwa wakilalamika na kupanga kuifikisha Tume mahakamani.
3. **Wanajeshi katika Makambi ya Jeshi na JKT:** Tume kwa kawaida haiweki vituo katika Makambi ya Jeshi, Polisi na Magereza. Kutokana na programu maalumu za baadhi ya vikosi Jeshi liliomba kuwepo utaratibu maalumu la Kuwaandikisha
4. **Wananchi Waliopo Magerezani:** Tume ilipata barua kutoka Magereza ikiomba kuwepo na utaratibu wa kuwaandikisha Wafungwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
5. **Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:** Bunge la Bajeti lilipokuwa linaendelea na vikao vyake Tume ilipata maombi ya kwenda kuwaandikisha Wabunge Dodoma.

Kama inavyonekana makundi mbalimbali yaliomba kuwepo utaratibu maalumu wa kuandikisha makundi hayo. Kutokana na muda uliopo itakuwa vigumu kuwa na Utaratibu wa kuandikisha kundi lolote kati ya

hayo ingawa inaonekana dhahiri kuwa Kundi la Wakimbizi na Wanafunzi wa Dar es Salaam lingeweza kufikiriwa kuadikishwa kulingana na Ratiba ya Display.

Aidha katika kikao cha Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa ilipendekezwa kutoandikisha katika Makambi ya Wakimbizi kwa madai kuwa itakuwa sawa na kuanzisha nchi ndani ya nchi hivyo kuhatarisha uasama wa Taifa. Baadhi ya Makambi yameonekana kuwa na Upande fulani kulingana na Itikadi za Vyama jambo ambalo Tume inaweza kulalamikiwa imepanga kuongeza za Chama fulani. Hivyo ilionekana ni vyema kusubiri hadi Wakimbizi hao waliopewa uraia watakapotawanywa maeneo mbalimbali.

Kwa upande wa Wanafunzi, iwapo watahitaji kuandikishwa, inawezekana Wanafunzi wote Tanzania wa Vyuo nao wakadai kuandikishwa jambo ambalo linaweza likaleta vurugu kwani BVR Kit zilizopangwa kutumika katika zoezi la Display ni chache na hakukuwa na Bajeti ya Uandikishaji baada ya siku za Uandikishaji zilizopangwa.